



DSPACE

<https://dspace.org/>

**Mapitiyo ya Windo Chungu cha Duncan Obwacha Kur.60.
Bestar Publishers LTD. ISBN 9702106174713: University
of Kabianga Donates Hand Sanitizers to Kericho County
Government**

Karama, Mohamed

2020-09

University of Kabianga

<http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/419>



ISSUE NO.4

The University of Kabianga Newsletter

ISO 9001:2015

Certified Institution

Quarterly Publication from the Office of the Vice-Chancellor

SEPTEMBER 2020

University of Kabianga donates hand sanitizers to Kericho County Government.



Prof. Wilson Kipngeno; Vice-Chancellor of the University of Kabianga (right on the photo) led the University team as Hon. Paul Chepkwony (left on the photo) receives Hand wash soap and sanitizers produced by the University's School of Science and Technology./Photo Nicholas Langat

Highlights

UoK donates Sanitizers

Editorial by new team

Confronting the Pandemic mentally

Vice-Chancellor's address.

THE UNIVERSITY DONATES SOAP AND SANITIZERS TO COUNTY GOVERNMENT OF KERICHO

The University of Kabianga community is privileged to be among those fighting Covid-19 by donating hand washing soap and hand sanitizers to the County

Government of Kericho. The University, in its quest to contribute to the fight against corona virus spread in Kericho County, donated three hundred pieces of hand washing soap and three hundred and fifty pieces of hand sanitizers. Besides, the University was at

an advanced stage of donating maize flour to, Africa Gospel Church (AGC) Baby Home in Nakuru County, Bethel Faith Home and Kipcham Gaa Children's Home both in Kericho County.

Conti..Pg 3

INNOVATION AND EXCELLENCE

**MAPITIYO YA WINDO CHUNGU
CHA DANCAN OBWOCHA,
KUR. 60., BESTAR PUBLISHERS
LTD. ISBN 9702106174713**

Nilikaa kusoma Windo Chungu katika mkao mmoja si kwa sababu ya kuwa ina sifa ya hadithi fupi bali ni kwa sababu nilikhiari kuwacha yoe siku hiyo bui niimalize hadithi yote kwa mara moja. Kilichoniweka kuisoma kwa mfululizo ni kwa kuwa hadithi imejaa msimko kutokana na ustadi wa matumizi mazuri ya taharuki mithili ya tatuzi za Bwana Msa. Kila ukifika kivuko kimoja unakivuka haraka ili utake kujuwa kuna nini mbele.

Hadithi yenyewe ni ya masikitiko, huzuni, na uchungu juu ya unyama anaofanyiwa mtu kwa kosa la mtu mwingine. Mzee Mabwocha alipojitiya na kujitowa kwenye makunri ya wachawi yalikuwa maamuzi yake mwenyewe; mwanawe Dante yuwahusika-je katika maasi ya babake? Walakini makunri haya yanayofanya mambo ya kiyajabu: ya kula nyama mfu za watoto wachanga, kudhuru na kusongonyowa aila ya wanachama wanapokataa kwenreleza kuwa wanachama, na kuwapa utajiri wa chapchap wote wanaokubaliyana na matambiko haya ni katika mambo aliyoyaangaziya mwandishi kwa kina.

"Nilishangaa sana kupata

nguvu ya ajabu na ya ghafla sana mbele ya Mukulungu ambaye aliogopwa na kila mtu" nriyo maneno sumaku yanayobadilisha yanayojiri baada ya uwamuzi huu "... na liwe liwalo". Madonroo haya ni mojawapo ya kauli anazotumiya mwandishi Obwocha kututaharukisha na kutuhamasisha wakati tunapokabiliwa na zani mbele yetu maishani. Anatushajiisha tusikubali kattu kutawaliwa na tamaa ya utajiri ambao rasilimali yake ni unyama juu ya binadamu wenzako. Hadi mwisho wa hadithi mwandishi anamfanya Dante aumiye kwa hali zote lakini asilbadili uwamuzi wake.

Mwandishi ametumiya lugha nyepesi yenye kauli fupifupi zisizo na utoziti mwingi, na kwa kutumiya ploti sahili ameweza kuifanya hadithi ishuke kwa utamu na iyeleweke kwa urahisi sana. Mwandishi ametumiya taswira pevu zenye hisiya kali zikiwamo mateso anayokumbana nayo Dante (mhusika mkuu) na mpenziwe Rita, matambiko na makafara wakati wa makongamano ya wachawi. Usukaji huu mwepesi unamfanya msomaji auhisi uchungu anawousikiya Rita kila anapoharibu mimba, na uchungu wa Dante kutoweza kubadilisha mkono wa mwenenro wa maisha yao.

Hata hivo, kazi hii ilinakisika,

bila kuharibu ladha, kwa makosa ya hijayi (k.m ni Mukulungu au Makulungu), upigaji chapa hobelahobela (kukosekana alama mwafaka za uwakifishaji), na matumizi ya 'sheng' (kujiingiza kwa mambo ya uchawi).

Ni kazi aali kwa wanafunzi wa madarasa ya juu katika shule za msingi kutokana na lugha ya utambaji hadithi. Piya itawafaa wanafunzi wa kiwango cha vyuo kutokana na ubainishaji wa mbinu nyingi za kisanii alizotumiya mwandishi hususani taharuki. Sina shaka msomaji yoyote wa kazi hii atasema, "Ama kwell Kabianga kumezalikana mkembe wa Mohamed Said Abdulla!"



**Dkt. Mohamed Karama
Idara ya Isimu Fasihi na
Mawasiliyano**

EDITORIAL BOARD

Dr. Robert Wesonga (**Editor-in-Chief**), Ms. Anne Tenya (**Editor**), Ms. Jacqueline Kandagor (**Content Editor**), Mr. Nicholas Langat (**Secretary/Editor**) and Mr. Eliud Lilan (**Design & Layout**)

The University of Kabianga Newsletter is Published by the Office of the Vice-Chancellor.

The Editorial Board Welcomes brief comments, articles or news on topical issues.

send to corporateaffairs@kabianga.ac.ke